# Ifahamu

CRDB BANK

# Kijani Bond

1. **Hati Fungani ni nini?**
Hati fungani ni aina ya uwekezaji ambapo mwekezaji anawekeza pesa zake katika taasisi (shirika au serikali) kwa muda maalum na kisha kupata faida kutokana na uwekezaji wake.

2. **Nini tofauti kati ya kuwekeza katika hati fungani na kuweka fedha katika akaunti ya muda maalum?**
• Unapowekeza katika hati fungani, unaikopesha fedha zako benki/taasisi inayotoa hati fungani. Hivyo, unakuwa hauweki fedha katika akaunti ya mteja.
• Hati fungani ya CRDB inaweza kuuzwa katika soko la hisa la Dar Es Salaam (DSE) kabla hata ya ukomavu wake na mshika hati fungani/mwekezaji atalipwa kiasi cha awali na faida yoyote iliyolipwa hadi muda huo tofauti na akaunti ya muda maalum.

3. **Kijani Bond ni nini?**
Kijani Bond ni aina ya uwekezaji wa hati fungani ambapo fedha zinazokusanywa ni kwa ajili ya miradi rafiki kwa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia-nchi.

4. **Mteja anapata Faida gani akiwekeza katika Kijani Bond?**
**Kwa kuwekeza katika Kijani Bond, mwekezaji/mteja atapata:**
(i) Usalama wa fedha katika kipindi chote cha uwekezaji
(ii) Uhakika wa faida inayovutia katika kipindi kizima cha hati fungani.
(iii) Faida ya 10.25% kwa mwaka italipwa mara mbili kwa mwaka na sio hadi muda wa hati fungani kukomaa
(iv) Mteja /Mwekezaji hata katwa kodi kwenye faida atakayopata.
(v) Kuwa sehemu ya jitihada za ulimwengu za kukabiliana na mabadiliko ya tabia-nchi.
(vi) Ukihitaji fedha zako, kabla ya muda wa hati fungani kukomaa, unaweza kuuza hati fungani yako kwa wakala wa soko la hisa (DSE)
(vii) Utaendelea kunufaika na faida ya hati fungani hadi muda utakapouza hati fungani au muda wa ukomavu wa hati fungani.

5. **Faida ya Kijani Bond ni asilimia ngapi?**
Kijani Bond ina faida ya 10.25% kila mwaka. Inalipwa kila baada ya miezi 6 (nusu mwaka)

6. **Nani anaweza kuwekeza katika Kijani Bond?**
• Watu Binafsi (miaka 18 na Zaidi)
• Watoto (Kupitia mzazi au mlezi)
• Vikundi,
• Mashirika/taasisi,
• Raia na wasio Raia wa Tanzania.
• Uwekezaji wa pamoja; mfano mke na mume

7. **Ni kiasi gani Mwekezaji/Mteja anahitaji kuwekeza katika Kijani Bond?**
Kiwango cha uwekezaji ni TZS 500,000 na kuendelea, hata hivyo Mwekezaji anaweza kuende lea kuongeza uwekezaji wa Kijani Bond kupitia wakala wa DSE.

8. **Mwekezaji/Mteja anajiungaje na Kijani Bond? Ili kuwekeza katika Kijani Bond,**
i. Mwekezaji/Mteja atajaza fomu ya maombi ya Kijani Bond iliyotolewa na tawi la CRDB au wakala wa hisa. Taarifa muhimu zinazopaswa kutolewa kwenye fomu:
    • Taarifa za Mwekezaji na anwani halisi
    • Taarifa za akaunti ya benki itakayopokea Faida na kiasi cha awali.
    • Akaunti ya CDS (kama hauna akaunti ya CDS utafunguliwa)

# Ifahamu

CRDB BANK

Kijani Bond

ii. Kitambulisho halali - Pasipoti, Leseni ya Udereva, Kitambulisho cha Taifa, Kitambulisho cha mpiga kura, Kitambulisho cha Zanzibar Mkaazi
iii. kuweka kiasi cha uwekezaji cha TZS 500,000 au zaidi kwenye akaunti ya CRDB iliyotajwa kwenye fomu ya maombi

**9. Kijani Bond inakomaa baada ya muda gani?**
Kijani Bond inakomaa baada ya miaka 5 (18 Oktoba 2028)

**10. Mwekezaji/Mteja atapokeaje Faida na kiasi cha awali cha uwekezaji katika Kijani Bond?**
Malipo yote yatafanywa moja kwa moja kwenye akaunti ya mwekezaji iliyotolewa katika fomu ya maombi ya Kijani Bond.

**11. Je, Mwekezaji/Mteja anaweza kujaza akaunti isio na jina lake kama akaunti ya kupokelea Faida?**
Hapana, mwekezaji/mteja anapaswa kuweka akaunti yenye majina yake sahihi.

**12. Mwekezaji/Mteja anaweza kuanza lini kuwekeza kwenye Kijani Bond?**
Ratiba ya awamu ya kwanza ya Kijani Bond ni kama ifuatavyo:

| TUKIO | TAREHE |
|---|---|
| **Kufunguliwa kwa mauzo ya Kijani Bondi** | **31 Agosti 2023** |
| **Kufungwa kwa ofa** | **06 Oktoba 2023** |
| **Tarehe ya kusajiliwa kwenye soko la hisa** | **27 Oktoba 2023** |
| **Ukomavu wa Bondi** | **18 Oktoba 2028** |

**13. Akaunti ya CDS ni nini?**
Akaunti ya CDS "inawakilisha" mfumo wa kumbukumbu ya elektroniki ambao unaweka kumbu kumbu za umiliki wa hati fungani zilizoshikiliwa na watu binafsi au taasisi na kurahisisha uhamisho wao. Mfumo huu unasimamiwa Dar-es-salaam stock exchange (DSE).

**14. Mwekezaji/Mteja anapataje Akaunti ya CDS?**
Iwapo Mwekezaji/Mteja hana namba ya akaunti ya CDS, itafunguliwa kwa kutumia taarifa zilizo jazwa na Mwekezaji/Mteja kwenye fomu ya maombi ya Kijani Bond.

**15. Je, Mwekezaji/Mteja anahitaji kuwa na akaunti ya benki na CRDB ili kuwekeza?**
Tunashauri mwekezaji/mteja kufungua akaunti na CRDB ambayo itarahisisha kupokea faida.

**16. Je, Kiwango cha Faida kinaweza kubadilika?**
Hapana, Kiwango cha faida (10.25% kwa mwaka) hakitobadilika katika kipindi chote cha uwekezaji.

**17. Mteja/Mwekezaji anawezaje kukokotoa kiasi cha faida atakayolipwa?**
Kikokotoo kinapatikana kwenye tovuti ya CRDB. https://crdbbank.co.tz/en
Mfano; Kijani Bond ya TZS 100M, itakayolipwa kwa miaka 5 kwa Faida ya 10.25% kwa mwaka.

# Ifahamu

| KIKOKOTOO CHA KIJANI BOND | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kiasi cha Hati Fungani | | | 100,000,000 | <<<<Ingiza Kiasi |
| Kiwango cha kuponi kwa mwaka | | | 10.25% | |
| | Idadi | Mwezi | Kiasi cha kuponi-kila miezi sita | Kiasi cha kuponi kila mwaka |
| **1** | 1 | 6 | 5,125,000 | 10,250,000 |
| | 2 | 12 | 5,125,000 | |
| **2** | 3 | 18 | 5,125,000 | 10,250,000 |
| | 4 | 24 | 5,125,000 | |
| **3** | 5 | 30 | 5,125,000 | 10,250,000 |
| | 6 | 36 | 5,125,000 | |
| **4** | 7 | 42 | 5,125,000 | 10,250,000 |
| | 8 | 48 | 5,125,000 | |
| **5** | 9 | 54 | 5,125,000 | 10,250,000 |
| | 10 | 60 | 5,125,000 | |
| | Jumla | | 51,250,000 | 51,250,000 |
| **Jumla Kuu (Kiasi cha awali + Faida)** | | | | **151,250,000** |

**18. Je, Kijani Bond inapatikana kwa sarafu za kigeni?**
Kwenye awamu ya kwanza Kijani Bond inapatikana kwa Shilingi ya kitanzania pekee. Iwapo mteja ana fedha za kigeni atalazimika kuzibadilisha kupata shilingi ili kuwekeza kwenye Kijani Bond.

**19. Je, Mteja wa Kijani Bond anaweza kusitisha uwekezaji kabla ya tarehe ya ukomavu?**
Hapana, uwekezaji ni kwa kipindi cha miaka 5. Iakini, mwekezaji anaweza kuuza sehemu au kiasi chote kwenye soko la hisa la DSE.

**20. Je, Mwekezaji/Mteja anaweza kuwa na Kijani Bond zaidi ya moja?**
Mteja anaweza kuwekeza kwenye hati fungani mara moja. Iwapo mwekezaji anataka kuongeza uwekezaji katika Kijani Bond, anaweza kununua kwenye soko la hisa la DSE kupitia mawakala waliothibitishwa.

**21. Iwapo mmiliki wa Kijani Bond amefariki nini kitatokea?**
Umiliki wa Kijani Bond utahamishiwa kwa mrithi wa mali za marehemu aliyeidhinishwa kisheria.

**22. Je, Mwekezaji/Mteja atapata cheti cha umiliki wa hati fungani?**
Ndio, Mteja/Mwekezaji atapata cheti cha umiliki hati fungani.

**Kwa maelezo au maswali ya ziada tafadhali wasiliana na sisi kupitia;**
Barua Pepe: info@crdbbank.co.tz
Namba ya simu: +255(22)2197700 | +255(0)714197700 | +255(0)755197700 | 0800008000